PHOTO: NARENDRA PATEL

BINTI UYUNI MUSSA

na
PETER KILEMBA

BINTI Uyuni Mussa akiwa mzalia wa Mvita Kenya umri wa miaka 21, alisoma huko shule ya Mvita na hatimaye kuendelea na mafunzo va vidato shule ya New Era mjini Mombasa, ambako alishiriki katika uandishi wa michezo na kutwaa nafasi ya kushiriki katika michezo akianzia shule hiyo. Kufunguliwa kwa Stesheni ya Mombasa ya Television kulimpa moyo kujitokeza uwanjani na akawa mara kwa mara akijulikana kwa jina la Chiriku. Afahamuye lugha 'Chiriku' ni aina ya ndege mpenda kuimba ama kuongea, naye Uyuni alikuwa chiriku wa lugha katika Sinema ya television kutoka Mvita.

Alishiriki katika vipindi vingi kama vile kipindi cha *Fedheha* na hivi sasa ni mmoja wapo wanaosimamia kipindi kipya kijulikanacho kwa jina la *Ndowano*. Lakini hatujui ndowano hiyo ina lengo gani.

* * * * *

RAIS MOI APONGEZWA

na
S. A. AL-ISMAILLY

MAMILLIONI ya wananchi wa Kenya wa tabaka zote za maisha wamempongeza Mtukufu Rais Daniel Arap Moi kwa hatua zake alizotwaa wakati wa kuadhimisha Sikukuu ya Jamhuri mnamo Disemba 12 mwaka huu.

Rais Moi alipohutubia Taifa la Kenya alitoa miongozo thabiti yenye lengo la kudumisha UMOJA wa Taifa , AMANI ya Taifa la Kenya na MAENDELEO ya Taifa la Kenya.

Lengo hili thabiti la Rais Moi limethibitisha msingi mwema wa Taifa hili la Kenya uliowekwa na Muanzilishi Hayati Rais Mzee Jomo Kenyatta.

KUFUNGULIWA WANASIASA

Wananchi wa pande zote za Jamhuri wamempongeza Rais Moi kwa hatua yake ya busara ya kuwaachilia huru wanasiasa wa Kenya ambao wamekuwa vizuizini.

Hatua hiyo imedhihirisha imani ya Rais Moi kuwahurumia wale waliokuwa vizuizini na ni wajibu wetu kudumisha yale yalio mema kwa taifa la Kenya na kuepukana na mabaya ambayo yanaweza kuhatarisha UMOJA wa Taifa, AMANI ya Taifa na MAENDELEO ya Taifa.

Mambo haya matatu yalitiliwa mkazo na Rais Moi kwa faida ya wananchi wote wa Kenya na vizazi vyetu vijavyo, na LAZIMA kuhifadhiwa, na kwamba AMANI na UMOJA wa Taifa hili ndio msingi ambao umeipatia Kenya sifa, maendeleo ya kutajika na Umoja wa wananchi.

SI NDOTO LENGO LA RAIS MOI

Rais Moi yuwatekeleza kwa vitendo, vitendo vya kuonekana kwa macho na kudhirika kila upande. Haikuwa ndoto kuumaliza ufisadi wa shughuli za KIMAGENDO ambazo zilihatarisha taifa la Kenya, uchumi wa taifa na maendeleo ya taifa.

Rais Moi ameonesha kwa watu wake kwamba lengo lake ni Kenya wala si kundi au watu binafsi. Mungu atamsaidia wakati wananchi wote wa Kenya wakiwa pamoja naye katika juhudi zake za kuleta ufanisi mkubwa zaidi kwa Taifa na watu wa Kenya.

MTUKUFU RAIS DANIEL ARAP MOI

Rais Moi ametangaza elimu ya Bure mpaka darasa la Sita kote nchini hatua ambayo ina lengo la kupambana na kutojua kusoma na kuandika. Elimu ndio muangaza, taa ya kilimwengu, na Rais Wetu ametwaa hatua ya kuona kwamba kila mtoto anayefikia umri wa kwenda shule, atakwenda shule bila kizuizi ama sababu yo yote.

Akitangaza kutolewa kwa MAZIWA ya BURE katika shule za msingi mwakani tamu ya pili mwaka ujao, Rais Moi amekuwa na lengo la kuona kwamba wanafunzi wa Kenya wanapata chakula cha kujenga Miili yao, hatua ambayo imefurahiwa na maelfu ya wananchi wa Kenya ambao maziwa baadhi ya wao huwa ni tunu kubwa au chakula cha kutumiwa na wenye uwezo.

NAFASI ZA KAZI

Hatua za busara za Rais Moi kuongeza kipimo cha kazi kwa kumi kwa mia baada ya mashauri yake na Matajiri, hali kadhalika imefurahiwa na umati wa wananchi wa Kenya.

Alitoa mwito kwa vyama vyawafanyi kazi kufahamu hatua hiyo muhimu ili kuwawezesha wingine kupata nafasi za kazi na kuweza kudiriki maisha yao kazini.

ULINZI KWA WATU WOTE

Rais Moi alitoa hakikisho lake la kila mara kulinda kila mwananchi wa Kenya na mali za watu wa Kenya na wingine humu nchini na kuwa Taifa lenya intidhamu.

Alisisitiza juhudi na kazi zitakazoendelezwa na serikali yake katika kila sehemu ya taifa la Kenya.

PWANI YAMPONGEZA RAIS MOI

Viongozi wa siasa, jamii na wingine kote Pwani wamempongeza Rais Moi kwa hatua alizotwaa wakati wa kuadhimisha Sherehe za Jamhuri mwaka huu.

Wanasiasa wa Mombasa, wakiongozwa na Mwenyekiti wa Kanu Bwana Shariff Nassir wamempongeza Rais Moi kwa hatua ambazo zina lengo la kushaidisha UMOJA, AMANI na MAENDELEO ya taifa la Kenya.

PHOTO: NARENDRA PATEL

MKUU wa Mkoa wa Pwani Bwana Eliud Mahihu anaonekana akisoma hutubu ya Rais Moi kwa umati mkubwa wa wananchi wa Mombasa waliyohudhuria sherehe za Jamhuri katika kiwanja cha michezo cha manispaa ya Mombasa.

Sherehe hizo hali kadhalika zilihutubiwa na wabunge wa Mombasa pamoja na Mweneykiti wa Kanu Bwana Shariff Nassir ambaye pia ni Mbunge wa Mombasa ya kati.

Kati ya wageni waliyohudhuria sherehe hizo alikuwa waziri katika afisi ya mwenyekiti wa baraza la Mapinduzi kutoka Zanzibar Ndugu Haji Mfinde akiandamana na mwanachama wa baraza la Mapinduzi Ndugu I. K. Makungu

Coastweek *** JEMBE

SWAHILI CROSSWORD *No. 5*

JEMBE
UNGA SAFI NO. 1
WA MAHINDI



KWENDA KULIA:

1 Jina la Kistanu
3 Nduguye baba mwanamume
7 Nusu ya mama
9 Vuta pumzi
11 Gazeti mashuhuri la Pwani
14 'Halawa' herufi moja ina Makosa
16 Wa zamani
21 Kukutanika pamoja kanbu karibu
23 Kutia paa la nyumba
24 Kinyume cha p.m.
25 Weka npe
26 Ati

KWENDA CHINI:

1 Auogopa
2 Stesheni tulani Kenya
4 Mtoto wa nduguyo wa kike
5 Itoe roho inyonge
6 'Laki' imepungua herufi moja
8 Kaidi, vunja amri
10 Chipua, ota
12 Fanya arusi
13 Kupandisha kama bendera au tanga
15 Ukavu, hali ya ardhi isiyo na maji
16 Chuma ule uvulini
17 Kitongoji karibu ya Tanga
18 Sehemu, fungu
19 Kaza kwa meno
20 United Nations
21 Utupi wa Sasa Pika Sima
22 Coco

Washindi wa Fumbo La Kujaza Maneno No. 3:

(1) Mohamed Abdalla wa Sanduku la Posta 98702, Mombasa
(2) Athman J. K. Mwabungo wa Sanduku la Posta 10, Ukunda

MAJIBU YA SHINDANO LA FUMBO LA KUJAZA MANENO NO. 3

KWENDA KULIA:
1 UNO 4 PETE 8 MENO, 10 DUME, 12 ANJU, 13 AMBA, 14 EAMB, 16 AER 18 AUA, 20 ALIA, 23 ANUA, 26 WALE, 28 CHEE, 30 AMBA, 31 AUTU, 33 IEI

KWENDA CHINI:
1 UMA, 2 NENE, 3 ONJA, 5 EDA, 6 TUMA, 7 EMBE, 9 OUMA, 11 EARS, 15 BUA, 17 BAWA, 19 ANGA, 21 DAMU, 22 ALIA, 24 UHAI, 25 ALLE, 27 LAI, 29 EII

Shindano la fumbo la kujaza maneno:

Uamuzi wa majaji utakuwa wa mwisho. Hakuna malalamiko yoyote yatakayokubaliwa.

Washindi wawili wa kwanza kila mmoja atapatiwa bandali moja la Unga Wa Mahindi chapa Jembe.

Shindano hili limedhaminiwa na COASTWEEK LTD., pamoja na ATTA LTD., Mombasa.

Jawabu za fumbo hili, lipelekwe kwa muhariri COASTWEEK, sanduku la posta 87270, Mombasa, Kenya, siku ya Alhamisi tarehe 21.12.78, saa sita mchana shindano hili litakuwa mwisho.

KWA UFUPI

MKUU wa wilaya ya Mombasa, Bwana E. G. Karanja ametoa mwito kwa wakaazi wa Mombasa kuuchagia kwa ukarimu Mti wa Christmasi mwaka huu. Alisema ile dansi ya kuadhimisha Christmasi mwaka huu sasa itafanywa huko Oceanic Hotel mnamo tarehe Disemba 23.

*

NAIBU waziri wa Utalii na Mbuga za kuhifadhi wanyama wa Pori Bwana Clement Lumembe amewa shauri wenye Mahoteli na wanaosimamia safari za watalii kuona kwamba mipango ya kutoa 'Vocha' kwa watalii wakiwa nje ya Kenya udumishwe kwa kuhakikisha kwamba pesa zilizolipwa zinafika nchini Kenya bila udanganyifu wo wote. Alisema watumishi wa Mahoteli ni lazima kutendewa mema kama vile wanavyotenda mema katika kazi zao. Bwana Lubembe alikuwa akihutubu katika karamu moja huko Mombasa Beach Hotel. Aliwashauri wavuvi wa Pwani kushiriki katika vyama vyao vya shirika.

*

VIONGOZI wa Luo Union (Pwani) wamekata shauri kwamba mwaka 1979 utakuwa mwaka wa juhudi za pamoja za umoja wao za kukusanya pesa za kulipia deni linalodaiwa na Kampuni ya Pan African Insurance kuhusu malipo ya Ujenzi wa Tom Mboya Memorial Hall.

Akitangaza haya mwenyekiti wa Luo Union tawi la Mombasa Bwana Amimo alisema Kampuni ya Pan African Insurance ilitoa shillingi 540,000/- wakati wa ujenzi wa ukumbi huo wa kumkumbuka Marehemu Bwana Tom Mboya na mpaka sasa ni shillingi 199,000 tu zilizolipwa na zilizobaki ni shillingi 525,848/90 bado kulipwa. Alisema kwamba Kampuni ya Pan African imetisha kwamba ikiwa deni hiyo haitalipwa kufikia tarehe 16 January mwaka ujao Jumba la Tom Mboya litanadishwa hadharani ili kupatikana pesa za kulipa deni.

*

WAKAAZI wa Mombasa wamepongeza Mkuu wa Mkoa wa Pwani Bwana Mahihu kwa kuamuru Halmashauri inayosimamia mji wa Mombasa kuwatafutia nafasi watoto wa Mombasa wapato 1,500 ambao huenda wakakosa nafasi ya mafunzo ya darasa la kwanza mwaka ujao kwa upungufu wa madarasa.

HEKKO NAKUPA MTUKUFU RAIS MOI

na
SAIDY HAMADY LUNDO

Hekko nakupa kwa hilo
Kupinga Jambo ambalo
Jambo lituumizalo
Rais Kuligunduwa

Nawapige lolo-lolo
Rais kazana nalo
Magendo walipendalo
Rais Kaligunduwa

Tafuta na jenginelo
Nahaswa ikiwa silo
Wewe wakomeshe nalo
Rais kaligunduwa

Rais mwenye Muruwa
Nchini likituuwa
Sasa umeligunduwa
Jambo lituumizalo

Shauri zao ikiwa
Jambo hili kuliuwa
Karibu wataghumiwa
Jambo lituumizalo

Rais wetu chaguwa
Usiridhie likawa
Nchi ipate kupowa
Jambo lituumizalo

Baba fanya ufanyalo
Ukomeshe Chimbi lolo
Wazuiye watakalo
Rais kaligunduwa

Sheikeni Muambiwalo
Sajini na Makoplo
Musihadaiwe kwa mlo
Rais Kaligunduwa

Tamati Moi kwa hilo
Ukiona jambo ndilo
Napindi likiwa silo
Rais Kaligunduwa

Bora liwe na usawa
Wazuzi wakuzuzuwa
Magendo yatapunguwa
Jambo lituumizalo

Walinzi wahishimiwa
Musiwe mwahadiwa
Mirija ikapagawa
Jambo lituumizalo

Umezumbuwa khatuwa
Lipe moyo wa kukuwa
Nakuruhusu Bomowa
Jambo lituumizalo